**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**

Mkoa wa Kagera
Mtaa wa Pwani
S.L.P 1138
35111BUKOBA
Barua pepe:rbckagera@pccb.go.tz
TANZANIA
w.w.w.pccb.go.tz

**KAGERA – APRILI, 2022**

# UFUATILIAJI WA MIRADI YA MAENDELEO YA SHILINGI BILIONI 7.4 WAFANYIKA KAGERA NA KUANZISHA UCHUNGUZI DHIDI YA MIRADI TISA.

## 1.0 UTANGULIZI

**Ndugu wanahabari,**
Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa **(TAKUKURU)** Mkoa wa Kagera tumeendelea kutekeleza majukumu yetu kama yalivyoainishwa katika Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, namba 11 ya Mwaka 2007. Katika utekelezaji wa majukumu yetu tumeendelea kushirikiana na wadau wa mapambano dhidi ya Rushwa wakiwemo waandishi wa habari, viongozi wa Serikali na Vyama vya Siasa, Mashirika, Kampuni binafsi na wananchi kwa ujumla. Majukumu haya yametekelezwa katika wilaya zote za Mkoa wa Kagera ambazo ni Bukoba, Misenyi, Karagwe, Kyerwa, Ngara, Biharamulo na Muleba.

Katika kipindi cha miezi mitatu (**01/1/2022** hadi **31/03/2022),** TAKUKURU Mkoa wa Kagera tumeweza kufanya kazi zifuatazo:

## 2.0 UZUIAJI RUSHWA

**Ndugu wanahabari,**

Katika jukumu la Uzuiaji Rushwa tumefanya **tafiti nane (8)** katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kagera na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo **ishirini na nane (28)** yenye thamani ya zaidi ya **shilingi Bilioni saba (Shs 7,428,734,552.51).**

Miradi tuliyoifuatilia ni ya ukarabati wa miradi ya maji, ujenzi wa Hospitali, vituo vya afya, zahanati pamoja na ujenzi wa madarasa chini ya Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano Dhidi ya Uviko 19. Tafiti hizo na ufuatiliaji ulilenga kuthibitisha thamani ya fedha (Value for Money) katika utekelezaji wa miradi hiyo pamoja na kubaini mianya ya rushwa ili kuwa katika nafasi nzuri ya kushauri namna ya kuziba mianya hiyo.

- Katika miradi iliyofanyiwa ufuatiliaji, ipo miradi iliyobainika kuwa na mapungufu ikiwemo ya kutumia vifaa vyenye ubora tofauti na ilivyoelekezwa na BOQ. Kutumia kioo cha 4 mm badala ya 5mm; Uwekaji mbaya wa vigae (Tiles) kutokana na usimamizi hafifu wa kihandisi; Viti kutengenezwa pungufu na ilivyokadiriwa kwa maelezo kuwa fedha hizo hazikutosha; pia kutoweka kumbukumbu za utoaji wa vifaa kutoka stoo na ukiukwaji wa sheria na kanuni za manunuzi. Vilevile tulibaini uwepo wa urushwaji wa bei kwa baadhi ya vifaa vya umeme na ujenzi kuuzwa kwa bei kubwa kuliko bei ya soko. Vifaa hivyo ni kama mirunda na mbao.

Baada ya ufuatiliaji huu, imetolewa elimu kwa wahusika wa miradi saba **(7)** ili kuboresha kasoro zilizojitokeza na tayari maboresho yanafanyika. Miradi tisa **(9)** uchunguzi wa kina unaendelea kufanyika na Miradi kumi na mbili (12) kati ya 28 haikuwa na kasoro na hivyo inaendelea kukamilishwa.

## 3.0 UCHUNGUZI

Tumepokea jumla ya malalamiko mia moja sitini na nne (164) Kati ya malalamiko hayo, malalamiko **themanini na tisa (89)** yalikuwa ni malalamiko yasiyohusu rushwa, hivyo walalamikaji walielimishwa na kupewa ushauri na hakukuwa na taarifa iliyohamishiwa idara nyingine.

- Malalamiko **(75)** yalihusu rushwa na kufunguliwa majalada ya uchunguzi. Kati ya majalada hayo **75,** uchunguzi wa majalada 3**6** umekamilika na hatua mbalimbali za kisheria zinatarajiwa kuchukuliwa dhidi ya watuhumiwa. Majalada **39** uchunguzi wake bado unaendelea.
- Ida zinazolalamikiwa kutokana na taarifa **164 ni** Halmashauri (108); Idara ya fedha 45, Idara ya Elimu 10, Maendeleo ya jamii 9, ugavi 16, maji 6. Idara ya Afya 19 na Watendaji wa kata na vijiji 3. Taarifa zingine **56** zilihusu watu binafsi 10, taasisi za kifedha 5, mashirika binafsi (NGO) 4, Polisi 13, Uhamiaji 7, Mahakama 6, TANESCO 6 na Chama kikuu cha Ushirika Karagwe 5.
- Mashauri mapya **sita (6)** yalifunguliwa mahakamani na kufanya jumla ya mashauri **hamsini na moja (51)** yanayoendelea kusikilizwa mkoani Kagera.
- Mashauri manne yametolewa maamuzi ambapo mashauri mawili tumeshinda na mawili tulishindwa. Hatua za kukata rufaa zinaendelea kwa kuwa hatukuridhika na maamuzi yaliyotolewa.

## 4.0 UELIMISHAJI UMMA

Ili kuongeza uelewa wa wana Kagera katika mapambano dhidi ya rushwa msisitizo wetu umekuwa katika kutoa elimu katika makundi mbalimbali yenye kuhamasisha wananchi kutambua madhara ya rushwa, pamoja na namna ya kuzuia na kupambana na rushwa katika maeneo ya kazi na biashara, lengo likiwa ni kuifanya jamii ifahamu maana ya rushwa, vyanzo vyake na madhara yake katika jamii na kushiriki kikamilifu katika mapambano haya. Elimu kwa wananchi imetolewa kwa kutumia njia mbalimbali zifuatazo:

- Tumeshiriki katika vipindi mbalimbali kupia Radio Kasibante, Kwizera, Rumuli, Fadeco , Online Tvs nk

- Semina (49); Mikutano ya hadhara 52 kwa utaratibu wa TAKUKURU INAYOTEMBEA; Kushiriki maonesho 9 na pia tumeelimisha kwa kupitia Sanaa za maonyesho kwa utunzi wa Nyimbo, Mashairi, Ngonjera na uchoraji wa vibonzo vilivyoshirikisha wanachama wa klabu za wapinga rushwa mashuleni.

## 4.1 USHIRIKIANO NA WADAU

### 4.1.1 Ushirikiano wa TAKUKURU na Chama cha Skauti Tanzania - TAKUSKA

TAKUKURU Mkoa wa Kagera tumeimarisha ushirikiano baina yetu na Chama cha Skauti Tanzania kwa kutoa Elimu ya Mapambano dhidi ya rushwa kwa Skauti katika wilaya zote na kusajili wanachama wapya zaidi ya 400 katika Mkoa mzima.

- Tumeshiriki upandaji wa miti 3,000 katika shule za Sekondari za Kashozi miti 1,400, Katale miti 200 na Kalema miti 1,400.
- Skauti wa Shule za Sekondari za **Omumwani, Kashai, Kahororo, Kagemu, Kibeta, na Ihungo** wameshiriki katika shindano la utunzi wa masashairi, nyimbo, Ngonjera na uchoraji wa vibonzo ili kuwajengea Wanachama wa Skauti uelewa zaidi na ujasiri wa kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kutumia sanaa na kutoa elimu kwa jamii nzima.

### 4.1.2 Wanafunzi wa shule za Msingi, Sekondari na Vyuo Kupitia KLABU ZA WAPINGA RUSHWA

Kwa sasa tuna klabu za wapinga rushwa takriban katika shule zote za Msingi, Sekondari na Vyuo vilivyoko katika Mkoa wetu na tuna wachama zaidi ya 76,000. Tumelenga kuendelea kushirikisha kundi la vijana kwani tunaamini kuwa vijana ni hazina na rasilimali muhimu ya Taifa na ni chimbuko la mabadiliko na nguvu kazi ya Taifa.

## 5.0 **MAADHIMISHO YA WIKI YA SHERIA**

**Ndugu wanahabari,**

Katika maadhimisho ya wiki ya Sheria nchini TAKUKURU Mkoa wa Kagera ilitoa elimu kwa kugawa vipeperushi, majarida kwa wananchi waliofika katika banda la TAKUKURU.

## 6.0 MAADHIMISHO YA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI MACHI 8, 2022

**Ndugu wanahabari,**

Katika Mkoa wa Kagera maadhimisho hayo yalifanyika kimkoa katika Wilaya ya Misenyi ambapo TAKUKURU Mkoa wa Kagera tulishiriki kwa kugawa machapisho 768 (vipeperushi na majarida) na pia tulielimisha umma kuhusu rushwa ya ngono na madhara yake.

## 7.0 VIPAUMBELE KWA KIPINDI CHA APRILI – JUNI 2022

**Ndugu Wanahabari**

Pamoja na utekezaji wa majukumu yetu ya kawaida pia tumejiwekea malengo ya kutekeleza vipaumbele vifuatavyo vinavyolenga KUZUIA VITENDO VYA RUSHWA VISITOKEE:-

I. Kuongeza kasi ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ili kuziba mianya ya rushwa na ufujaji. Pia kama mtakumbuka, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania **Mhe. Philip Isdor Mpango**, wakati alipokuwa akihutubia wananchi katika Viwanja vya Mashujaa (Maarufu kwa jina la Viwanja vya Mayunga) vilivyopo katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba siku ya tarehe 18.3.2022 alisema. **Ninanukuu**

***"Bado kuna shida kwenye udhibiti wa mapato ya ndani ya fedha zinazokusanywa na Halmashauri zetu. Ni jukumu la viongozi kuvitambua vyanzo vyote na kutafuta namna bora ya kudhibiti mapato yote yanayotokana na vyanzo vya ndani ili kuziwezesha Halmashauri kuwa na uwezo wa kifedha. Pia tunatakiwa kuendelea kusimamia fedha za miradi ya maendeleo zinazoletwa***

***kwa kudhibiti urushwaji wa bei ili thamani ya fedha ionekane".*** Mwisho wa kunukuu.

Kauli hii imetuongezea ari na kasi ya ufuatiliaji wa miradi yote ya maendeleo ili kuhakikisha thamani ya fedha inaonekana, pamoja na kuendelea kudhibiti mapato yote yanayotokana na vyanzo vya ndani vya Halmashauri zote za Mkoa wa Kagera

II. Kuongeza kasi ya uelimishaji umma kwa kutumia njia mbalimbali.

III. Kuongeza kasi katika kufanya chambuzi za mifumo hasa katika maeneo yanayolalamikiwa zaidi.

**IV.** Tutaendelea kuelimisha jamii na hususani kundi la vijana kupitia ushirikiano uliopo kati ya TAKUKURU na SKAUTI – **TAKUSKA.**

## 8.0 HITIMISHO

**Ndugu wanahabari,**

Mapambano dhidi ya rushwa ni ya kila mwana Kagera, hivyo ili kuufanya Mkoa wa Kagera kuwa sehemu isiyokuwa na rushwa ni wajibu wa kila mmoja wetu kushiriki kikamilifu katika mapambano haya. Ninawashukuru wana Kagera wote ambao wamekuwa na wanaendelea kutoa ushirikiano kwa TAKUKURU. Pia kila mmoja wetu anahitaji kutanguliza maslahi ya nchi na kuchukua hatua katika kukabiliana na tatizo la rushwa katika Mkoa wetu.

Imetolewa na

signed

JOHN K.E JOSEPH

**MKUU WA TAKUKURU (M)**